

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA HAMSINI NA MBILI

21 JUNI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA HAMSINI NA MBILI – TAREHE 21 JUNI, 2023

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**681. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA
RAYMOND (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni nyumba ngapi zinahitajika kwa Watumishi wa Umma waliopo Vijijini.

**682. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Afya katika Kata za Mji wa Tarime kwa kuwa kuna Kituo kimoja tu cha Afya Nkende.

**683. MHESHIMIWA SYLVIA FRANCIS SIGULA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini SACCOS 130 za Wanawake na Vijana zitaanzishwa katika Mikoa 16 ikiwemo Kigoma kama ilivyoainishwa katika Ilani ya 2020/2025.

**684. MHESHIMIWA SILYVESTRY FRANCIS KOKA
(KIBAHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

- Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza eneo la ekari 1000 za Shirika la Elimu Kibaha.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**685. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY
(MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami Kilomita. 76 za Barabara ya Karatu - Mbulu.

686. MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA (NAMTUMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Mtwara Pachani – Nalasi hadi Tunduru utaanza.

WIZARA YA NISHATI:

687. MHESHIMIWA PROF. PATRICK ALOIS NDAKIDEMI (MOSHI VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, kuna mpango gani wa kupeleka nishati ya Gesi Asilia katika Vijiji vinavyozunguka Mlima Kilimanjaro ili kupunguza matumizi ya kuni.

WIZARA YA KILIMO:

688. MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutafuta masoko ya mazao ya kilimo.

689. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mkakati gani wa kufufua zao la Kahawa nchini.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

690. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha Tawi la Chuo Kikuu Huria katika Halmashauri ya Ifakara.

691. MHESHIMIWA JUDITH SALVIO KAPINGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kuna mkakati gani wa kudhibiti Watoto chini ya miaka saba kusoma Shule za Bweni.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

692. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, lini Serikali itaweka Kituo kidogo cha Forodha katika Kata ya Itiryo – Bikonge Tarime Vijijini.

**693. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMED
KUCHAUKA (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, lini Serikali itaifanyia mapitio Sheria ya Manunuzi ya Umma kwa kuwa ni kikwazo cha utekelezaji wa Miradi ya Halmashauri.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa likubali Kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
21 JUNI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**